أحكام النكاح - سواحيلي

# HUKUMU ZA NDOA




جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

هاتف: ٠١٦ ٤٢٣٤٤٦٦ ـ فاكس: ٠١٦ ٤٢٣٤٤٧٧

# HUKUMU ZA NDOA

## أحكام النكاح - سواحيلي

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات في الزلفي
هاتف: 966 164234466 ـ فاكس: 966 164234477

# HUKUMU ZA NDOA

## أحكام النكاح

### MASHARTI YA NDOA :

1. Kuridhia kwa wanandoa wawili : Haifai kutenzwa nguvu kijana aliefikia baleghe mwenye akili kuozeshwa mtu asie mpenda, wala kutevzwa nguvu binti kuozeshwa kijana asie mpenda, Uislamu umekaza mwanamke kuozeshwa bila ya ridhaa yake, na atakapo kataa kuolewa na mtu basi haifai kwa mtu yeyote kumuozesha kwa nguvu hata kama ni baba yake.

2. Waliyi : Ndoa haiswihi bila ya waliyi kwa kauli yake Mtume (saw) aliposema :

لقول النبي ﷺ : (( لا نكاح إلا بولي )) [رواه الترمذي: ١٠٢٠].

Mtume wa Allah anasema : ( Haiswihi ndo isipokuwa awepo waliyi) (Ameipokea Tirmidhiy : 1020).

Atakapojiozesha mwanamke mwenye, basi ndo yake ni batili sawa sawa ameifunga mwenyewe au amemuwakilisha mtu, wala hakuna uwaliyi wa mtu kafiri kwa Muislamu, na Kiongozi wa Dini ni Waliyi kwa yule ambae hana Waliyi.

Waliyi: Waliyi ni mtu aliebaleghe mwenye akili timamu anaetokana na ukoo wake kuanzia baba mzazi, kisha babu yake anaetokana na baba yake, kisha mwanae alie mzaa wa kiume au mjukuu wake wa kiume na kuendelea.

Kisha kaka yake wa tumbo moja, au kaka yake wa kuchangia baba, kisha watoto wa kiume wa kaka yake wa baba mmoja, kisha watoto wa ndugu yake aliechangia baba basi wa karibu na wa karibu zaidi.

Kisha a'mi yake baba na mama kwa baba yake, kisha A'mi yake aliechangia baba na baba yake, kisha watoto wa kiume wa a'mi zake na yule wa karibu na wakaribu zaidi, na hapana budi kwa Waliyi wa bint kumtaka idhini mwanamke kabla ya kumuozesha.

Na hikma ya kupatikana Waliyi ni kuziba njia ya zinaa, kwani mwenye kuzini hashindwi kumwambia mwanamke jiozeshe wenyewe kwa mahari kafulani, kisha washuhudilie watu wawili katika watu wake au watu wengineo.

3. Mashahidi wawili. Hapana budi kuhudhuria mashahidi wawili wanaume na zaidi waadilifu katika ufungwaji wa ndoa miongoni mwa waislamu.

Wawe ni wakweli walioepukana na madhambi makubwa mfano dhambi la uzinifu, kunywa pombe na mfano wake.

Na namna ya kufunga ndoa ni mtu kusema mwenye kuoa au muwakili wake katika kufunga ndoa: Niozeshe binti yako, au mtumwa wako Fulani na Waliyi atasema: Nimekuozesha binti yangu au mtumwa wangu Fulani.

Na atasema Mume nimekubali kumuoa, inaswihi kwa mwanamume kumuwakilisha mtu amtakae.

4. Ulazima wa mahari: ni vizuri kisheria mahari ikawa ni ndogo, na kila kinapokuwa kitu kidogo kikawa chepesi kinakuwa bora, na ni sunnah kuitaja mahari wakati wa kufunga ndoa.

Ikiwa mtu atampatia mkewe talaka kabla ya kumuingilia basi atachukua nusu ya mahari na ikiwa mwanamume atakufa kabla ya kumuingilia mkewe na baada ya kufunga ndoa mke huyo atamrithi mumewe na atachukua mahari kamili.

## ATHARI YA NDOA:

1. Kumlisha: Ni wajibu kwa mwananmume kumfanyia wema kwa kumlisha mkewe kwa kumlisha chakula, kumvisha nguo na kumpatia makazi ya kukaa, na atakapo mfanyia ubakhili katika jambo la wajibu atapata madhambi, na mwanamke ana haki ya kuchukua sehemu ya mali ya mumewe kiasi kinachomtosha katika chakula, na inamlazimu kutekeleza.

na chakula cha walima ni kile ambacho anakifanya mwanamume katika chakula siku za ndoa akiwaita watu kuja kula chakula hicho, nacho ni sunnah iliyoamarishwa kufanywa. Kwani mtume (saw) amefanya na ameamrisha kufanywa.

2. Kurithi: Muda mtu atakaofunga ndoa n mwanamke wa kiislamu ndoa sahihi basi muda huo kunapita kurithiana wawili hao pindi mmoja wao atakapo fariki dunia.

Alla (sw) anasema katika Quran:

لقوله تعالى: ﴿ وَلَكُمْ نِصْفُ مَا تَرَكَ أَزْوَاجُكُمْ ﴾ إلى قوله: ﴿ تُوصُونَ بِهَا أَوْ دَيْنٍ ﴾ [النساء: ١٢].

Allah anasema: (Mnayo nusu ya kurithi katika mali walizoacha wake zenu) mpaka kauli yake Allah (sw) (Mali uliyousia au deni) (An-Nisai : 12).

Hakuna tofauti ya kuwa alimuingilia, kujitenga au hakumuingilia.

## SUNNAH ZA NDOA NA ADABU ZAKE:

1. Ni sunnah kutangaza ndoa kama ambavyo ni sunnah kuwaombea wenye kufunga ndoa I kuwambia mume au mke mwenyezi mungu akubariki na akushuhie Baraka juu yako na awakutanishe katika kheri.

بارك الله لك وبارك الله عليك ، وجمع بينكما فى خير .

2. Ni sunnah kwa wawili hao wakitaka kufanya tendo la ndoa waseme dua hii :

(بسم الله. اللهم جنبنا الشيطان وجنب الشيطان ما رزقتنا)

(Ewe mwenyezi mungu tuepushe na shetani na ukiepushe na kile utakacho turuzuku).

3. Ni makuruhu kwa wanandoa wawili kuyatoa yale ambayo wanayo yafanya ndani katika mambo ya tendo la ndoa.

4. Ni haramu kwa mwanamume kumuingia mkewe hali ya kuwa yupo siku za hedhi au siku za nifasi hata kama atakuwa ametwaharika lakini ikiwa hajajitwaharisha kuoga.

5. Ni haramu kwa mwamume kumuingilian mkewe kinyume ya maumbile, na kufanya hivyo ni katika madhambi makubwa ambayo yameharamishwa na Uislamu.

6. Ni wajibu kwa mwanamume kumpatia mkewe haki yake kamili ya tendo la ndoa kama ambapo ni wajibu wakuto mwaga manii nje kwa kuchukia mwanamke kupata mimba isipokuwa kwa idhini ya mkewe au kwa dharura.

## SIFA YA MKE:

Ndoa inakusudiwa kustarehe na kutengeneza ukoo ulio mwema na jamii ilikuwa salimika, atakaposifika mwanamke na uzuri wa nje na ndani, lakini uzuri wa nje ni ukamilifu umbile, na uzuri wa ndani ni ukamilifu wa dini na tabia basi atakuwa amepata kheri kubwa, nako ni kukamilika na kufaulu kwa taufiq yake Allah, lakini jambo muhimu ni mwanamke mwenye dini kama alivyo tuusia mtume (saw) kwenye hilo, na pia ni juu yake mwanamke kumtafuta mwanamume mwema mcha mungu.

## WANAWAKE WALIOHARAMISHWA KUWAOA :

Wako wanawake wa aina mbili :-

1. Wako walio haramishwa kuwaoa milele nao wako aina tatu :

- Aina ya kwanza: Walioharamishwa kwa nasaba nao ni watu saba kama walivyotajwa kwenye Quran:

﴿ حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ أُمَّهَاتُكُمْ وَبَنَاتُكُمْ وَأَخَوَاتُكُمْ وَعَمَّاتُكُمْ وَخَالَاتُكُمْ وَبَنَاتُ الأَخِ وَبَنَاتُ الأُخْتِ... الآية ﴾ [النساء:٢٣].

(Mmeharamishiwa kuwaoa mama zenu, na mabinti zenu na dada zenu na shangazi zenu na ndugu wa mama zenu na mabinti wa ndugu zenu wa kiume na mabinti wa dada zenu…) (An-Nisai : 23).

i. Wanaingia katika mama: Mama mzazi, bibi sawa sawa upande wa baba au upande wa mama

ii. Binti anaingia binti uliemzaa na bint wa mtot wako wa kiume na binti wa binti yako wa kike, na wanavyoshuka.

iii. Dada wanaingia dada wa kuzaliwa nao baba mmoja na mama mmoja na dada wa kuchangia baba na dada wa kuchangia mama.

iv. Shangazi wanaingia shangazi wa baba mmoja na mama mmoja na baba yako, na shangazi aliechangia baba na baba yako na shangazi aliechangia mama na baba yako na shangazi wa babu yako na shangazi wa mama yako na shangazi wa bibi yako.

v. Dada wa mama yako wanaingia dada wa mama mmoja na baba mmoja na dada waliochangia baba na dada waliochangia babu mmoja na dada waliochangia mama mmoja na dada wa bibi yao mmoja.

vi. Binti wa kaka anaingia ndani yake binti wa kaka yako wa baba mmoja na mama mmoja na binti wa ndugu yako mliechangia baba na binti wa ndugu

yako mliechangia mama mmoja na mabinti wa watoto wao wa kiume na mabinti wa watoto wao wa kike na wanavyoshuka.

vii.Bint wa dada yako upande wa mama anaingia ndani yake mabint wa watoto wao wa kiume na mabint wa mabint zao na wanavyoshuka.

2. Walioharamishwa kwa kunyonya:
Nao ni wale wanaofanana na wale walioharamishwa kwenye nasaba mtume (saw) anasema:

« يحرم من الرضاع ما يحرم من النسب » [متفق عليه: ١٤٤٧،٢٦٤٥]

(Mtume wa Allah anasema: Wanaoharamishwa katika kunyonya ni wale wanaoharamishwa kwenye nasaba) (Ameipokea Bukhar na Muslim : 1447, 2645).
Kunyonya ambako kunakuwa haramu kuna masharti yake ambayo ni;
- Ni kunyonya mara tano na zaidi, atakapo nyonya motto kwa mama asiekuwa wake mara nne hatakuwa mama yake kwa kunyonya.
- Anyonye kabla ya kuachishwa, ni sharti awe amenyonya mara tano zote kabla ya kuachishwa kunyonya ikiwa ni baada ya kuachishwa au baadhi ya kunyonya baaba ya kuachishwa au baadhi ya kunyonya ni baada basi hatakuwa ni mama yake.
Ikiwa masharti yamekamilika basi atakuwa mtoto wa mwanamke, na watoto wake watakuwa ni ndugu

zake, sawa sawa wawe kabla yake au baada yake watoto watakuwa ni ndugu wa kunyonya, sawa sawa ni katika mama aliye aliye mnyonyesha au siye aliyemnyonyesha watakuwa ni ndugu zake, na hapa ni wajibu kijana kuwajua ndugu wa karibu wa aliye mnyonyesha ambao hawana mafungamano katika kunyonya na wala hawana athari ya kunyonya.

3. Walioharamishwa kwa Ukwe:

i. Wanawake asliolewa na baba, waliolewa na babu, wakati atakapofunga mtu ndoa basi anakuwa ni haramu kwa watoto wake kumuoa, na watoto wa watoto zao na watoto wa mabinti zao na kuendelea kushuka, sawa sawa amemuingilia au hakumuingilia.

ii. Wanawake wa watoto zao, wakati anapofunga kijana ndoa na mke, basi mke wake anakuwa haramu kwa baba yake na babu yake kumuoa na kuendelea, sawa sawa awe ni upande wa baba au upande wa mama kwa kufunga tu ndoa ni haramu, hata kama hajamuingilia.

iii. Mama mkwe na Bibi wa mke, atakapofunga mtu ndoa na mwanamke atakuwa huyo mama ni mama yake na bibi atakuwa ni bibi yake, kwa hiyo itakuwa ni haramu kuwaoa kwa kule kufunga ndoa, hata kama haja muingilia huyo mwanamke, sawa sawa

bibi awe ni upande wa baba kwa mkewe au upande wa mama kwa mkewe.

iv. Mabinti wa mkeo na mabinti wa mtoto wake wa kiume na mabinti wa mtoto wake wa kike na kuendelea, muda mtu anapomuoa mke na akamuingilia tu watoto wa mke wake hafai tena kuwaoa kwani wameshakuwa ni watoto wake, hafai kuwaoa watoto wa mtoto wake wa kiume na mabinti wa binti wa mke wake na kushuka ni haramu kwake, au ikipatikana kutengana kabla ya kumuingilia hapo patakuwa hakuna uharamu wa kumuoa mtoto wake.

2. Walioharamishwa kwa muda:

Nao ni aina zifuatazo;

i. Dada yake mkeo na shangazi yake mkeo, na ndugu wa mama yake, unaweza kuwaoa pale atakapo achika mke au atakapo kufa mke au atakapoachika mke na eda ikaisha.

ii. Mwanamke mwenye eda, atakapokuwa mwanamke yupo kwenye eda haifai kuolewa mpaka amalize eda yake, vile vile haifai kuposhwa akiwa ndani ya eda mpaka imalizike.

iii. Mwanamke alie hirimia hija au U’mrah, haifai kufunga ndoa mpaka amalize kabisa ibada hiyo na kuhalalikiwa na vile vilivyokuwa haramu kwake.

## TALAKA.

Asili ya talaka ni jambo la makuruhu halipendezi, lakini wakati mwingine hakuna budi kufanyika jambo hili, linaweza kumuudhi mwanamke kwa kubaki na mume au mume kubaki na mke.

Kutoka na rehma zake Allah (sw) kwa waja wake kukiwa kutatpatika kitu ambacho hakuna budi kuachana basi wanaweza kuachana kwa wema lakini ni wajibu kwa mwanamume kuchunga mambo yafuatayo;

1. Asimuache mwanamke akiwa hedhi, atakapo muacha mwanamke akiwa hedhi basi atakuwa amemuasi mwenyezi mungu na Mtume wake, na atakuwa amefanya kitu cha haramu itabidi huyo mwanamke amrudie na abaki nae mpaka atwaharike ndipo amuache au abaki naye akitaka, na ni bora ameache mpaka aingie hedhi ya pili atwaharike akitaka atambakisha na akitaka atampatia talaka.

2. Asimuache kwenye twahara ambayo alimuingilia, isipokuwa ikiwa imebainika mimba yake, ikiwa mwanamume ataamua kumuacha mke wake akawa amemuingilia baada ya hedhi, haruhusiwi kumuacha mpaka aingie hedhi kisha atwaharike hata kama itachukua muda mrefu akitaka atampa talaka lakini kabla ya kumuingilia, isipokuwa itakapobainika kuwa ana mimba, ikiwa anayo mimba anaweza kumpatia talaka.

## YANAYOENDANA NA TALAKA.

Talaka imekuwa ni kitenganisha cha mke, hakika kuna hukumu nyingi zinazoendana nazo miongoni mwazo ni;

1. Ulazima wa kukaa eda, ikiwa mtu amemuingilia mke wake, au akajitenga naye au akampa talaka kabla ya kumuingilia au kujitenga naye, basi hapo mke huyo hatakuwa na eda, na eda ni hedhi tatu ikiwa mke huyo ni katika wanawake wenye kuingia hedhi, na miezi mitatu ni kwa wale ambao hawaingii hedhi, na kujifungua ikiwa alikuwa na mimba eda inakuwa imeisha.

Na katika hikma za eda ni kumpatia fursa mume kumrejea mkewe vile vile kuhakiki kuwepo kwa mimba au kutokuwepo.

2. Ni haramu kwa mwanamke juu ya mume aliemuacha kabla ya hapo mara mbili yaani talaka mbili, alimuacha akamrudia ndani ya eda kisha akamuacha tena akamrudia kisha akamuacha tena mara ya tatu, itakuwa sio halali tena kwake mpaka aolewe na mume mwingine asiekuwa yeye ndoa iliyo sahihi, na amuingilie kisha amuache mwenyewe kwa hiari yake sio kwa kulazimishwa, baada yapo ndio huyu wa mwanzo anaweza kuwa halali kwake kwa kufunga ndoa nyingine.

Allah (sw) amemuharamishia mwanamke kwa aliye muacha talaka tatu kwa kuwahurumia wanawake kutokana na dhulma za waume zao.

## KHULU'U:

Khulu'u: Ni mwanamke kutaka kuachika kwa mumewe kwa kumchukia mume na kurejesha mali kumpatia mume ili ajitenge naye, lakini ikiwa aliyechukia ni mume ndie anayetaka kujitenga na mkewe basi haistahiki yeye mume kuchukua fidia. kwani ni juu lake kufanya subra au kuamua kumpa talaka.

Ni juu ya mwanamke kutotaka kujivua kwa mumewe isipokuwa atakapopata maudhi ya kufanya hivyo, maudhi ambayo hayawezekani kufanya subra juu yake, kama ambavyo haifai kwa mwanamume kumuudhi mkewe kwa makusudi mpaka akataka kujivua kwake, ni makuruhu kwa mwanamume kuchukua zaidi ya kile alichokitoa katika mahari yake.

## HIYARI KATIKA NDOA :

Inathibiti ndoa na kubakia katika mafungamano ya ndoa au kuharibika ndoa pale ambapo mmoja ya wana ndoa atakapopata sababu miongoni mwa sababu atakayoipata mume kwa mkewe au mke kwa mumewe kama vile maradhi, aibu ya kimaumbile

ambayo hakumbainishi mkewe kabla au hakumbainishia mumewe kabla au ikagundulika ndani ya ndoa, hapo atakuwa mmoja wao ana hiyari ya kubaki kwenye ndoa au kuivunja ndoa, mfano ;

1. Atakapokuwa mmoja wao ni mwenda wazimu au akawa mmoja wao amepatwa na kitu ambacho kinapoteza haki za mwingine kikamilifu katika ndoa, basi huyu mwingine ana haki ya kuivunja ndoa, lakini ikiwa atafanya hivyo kabla ya kuingiliwa basi mume atarejeshewa ile mahari aliyoitoa.

2. Ugumu wa kutoa mahari hapo hapo, mwanamke anayo haki ya kuvunja ndoa kabla ya kuingiliwa lakini baada ya kuingiliwa atakuwa hana haki kwenye hilo.

3. Ugumu wa kulishwa na kupata matumizi, kwa yule mwenye ugumu wa kumlisha mkewe, atasubiri mke kadiri atakavyoweza kisha anayo haki ya kuvunja ndoa kwa kupitia KADHI.

4. Atakapopotea mume hajulikani sehemu alipo na hakumuachia mkewe chochote katika chakula na wala hakuacha wasia kwa yeyote kumlisha mkewe, na hakuna mtu wa kumlisha mkewe, na mwanamke hana cha kujisaidia katika kupata chakula, basi mwanamke anayo haki ya kuvunja ndoa kwa kupitia KADHI kisheria.

## KUMUOA ASIYEKUWA MUISLAMU:

Ni haramu kwa muislamu kumuoa mwanamke kafiri asiekuwa Alhul kitabi, mwanamke wa kiislamu haifai kuolewa na mwanamume asiekuwa muislamu, sawa sawa awe ni Ahlul kitabi au asiwe Ahlul Kitabi, kama ambavyo haifai kwa mwanamke atakaposilimu kabla ya mumewe ajitulize kabla ya mumewe kusilimu.

Zifuatao ni baadhi ya hukumu za ndoa za wasiokuwa waislamu.

1. Watakapo silimu wasiokuwa waislamu (makafiri) mume na mke watabakia katika ndoa yao ile ile hakuna kizuizi cha kisheria kama vile kuwa mwanamke ni haramu kwa mumewe au mume sio halali kwa mkewe kwamba watenganishwe kati yao.

2. Atakaposilimu wanamke Ahlul Kitab watakuwa kwenye ndoa yao.

3. Atakaposilimu mmoja ya wanandoa wawili katika Ahlul Kitab kabla ya kumuingilia ndoa inabatilika.

4. Atakaposilimu mwanamke asiekuwa muislamu awe ni Ahlul Kitab au sio Ahlul Kitab kabla ya kumuingilia ndoa inavunjika kwani mwanamke wa kiislamu sio halali kwake kafiri.

5. Atakaposilimu mwanamke kafiri baada ya kuingiliwa itasimama amri juu ya kuisha eda, kwani ndoa itavunjika

baada ya kuisha eda ikiwa hatasilimu mume, hapo ataolewa na mume amtakaye, akipenda atasubiri mpaka mumewe naye asilimu lakini atakuwa mwanamke hana haki kwa yule mume kipindi hicho cha kusubiri kama vile ambavyo mume hana hukumu juu ya mke, akisilimu mume anakuwa ni mke wake bila ya kufunga ndoa mpya hata kama atasubiri miaka mingi, hivyo hivyo hukumu atakaposilimu mume asiekuwa Ahlul Kitab.

6. Atakaporitadi mwanamke akauacha uislamu kabla ya kuingiliwa ndoa inavunjika, wala hakuna mahari na hata kama mume ndie alieritadi itavunjika ndoa na ni juu yake kutoa nusu ya mahari, na atakaposilimu alieritadi kati ya wawili hao watakuwa katika ndoa yao ya mwanzo kwa kutopatikana talaka kati yao.

## ATHARI INAYOPATIKANA KATIKA NDOA ZA AHLUL KITABI:

Wakati Allah (sw) alipo halalisha ndoa lengo kubwa ilikuwa ni kuzitengeneza tabia, na kuisafisha jamii na uchafu na kuzihifadhi tupu na kusimamisha nidhamu ya uislamu iliyo sahihi katika jamii, na kuutoa ummah wa uislamu unao shuhudilia ya kwamba hakuna mola anaepasa kubudiwa kwa haki isipokuwa mwenyezi mungu mmoja tu, na Muhammad ni Mjumbe wa mwenyezi mungu, na hayapatikani haya masilahi isipokuwa kwa kuoa tu mwanamke mwema mwenye

dini, heshima na tabia njema, ama athari za muislamu kumuoa mwanamke Ahlul Kitabi tutaelezea kwa ufupi mambo yafuatayo;

1. NDANI YA FAMILIA: Ama ndani ya familia ndogo akiwa mume ni shupavu na mwenye nguvu katika usimamizi, basi ataleta athari kwa mke wake, na dhana kubwa mwanamke atakinaika na uislamu, na pia inaweza kupatikana kinyume ya hayo.

Anaweza kufuata mke akidhani kuwa ni mazuri katika dini yake, kama vile kunywa pombe, kula nguruwe na kufanya urafiki, kwa hali hii itaparaganyika familia ya kiislamu na watakua watoto wa kiislamu katika mambo mabayana watazidi katika mambo mabaya na atafanya kwa makusudi kuwalazimisha watoto kwenda nao kanisani na watazoea kuona swala za kinaswara na watakulia katika mazingira hayo.

2. ATHARI KATIKA JAMII: Kukithiri wanawake wa Kikiristo katika jamii ya kiislamu ni jambo hatari sana, kwani wao inakuwa ni sababu moja kubwa ya kupatikana vita vya kifikra ndani ya Ummah wa Kiislamu, kwa yale yanayosomwa kwa kuhalalisha na kupindisha katika yale wanayo yafuata katika desturi yao ya Kinaswara kila siku, ambayo ni kawaida wao kuchanganyika kati ya mwanaume na wanawake katika hali ya ukaaji uchi wa mavazi yao na baadhi ya kutilia mkazo katika kwenda kinyume na mafunzo ya Uislamu.

# FIHRISI YA KITABU

HUKUMU ZA NDOA: ........................................................ 3

MASHARTI YA NDOA :...................................................... 3

ATHARI YA NDOA:........................................................... 5

SUNNAH ZA NDOA NA ADABU ZAKE: .............................. 6

SIFA YA MKE:................................................................ 8

WANAWAKE WALIOHARAMISHWA KUWAOA : .............. 8

TALAKA. .................................................................... 13

YANAYOENDANA NA TALAKA........................................ 14

KHULU'U: .................................................................... 15

HIYARI KATIKA NDOA :................................................. 15

KUMUOA ASIYEKUWA MUISLAMU: .............................. 17

ATHARI INAYOPATIKANA KATIKA NDOA ZA AHLUL KITABI:................................................................. 18